

MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA MJINI MOSHI



DIRA YA MAJI

Usahihii wa Matumizi ya Maji ya Mteja ni jambo muhimu sana katika kudumisha uhusiano mzuri baina ya Mamlaka na Mteja wa maji. Kwa msingi huu, Mamlaka inalazimika kumfungia Mteja Dira ya Maji ili kupata kumbukumbu sahihi ya matumizi ya maji ya Mteja badala ya kuwa na ankara za makisio.

Dira ya Maji hufungwa kwa Mteja kwa masharti yafuatayo:

- **Dira ya Maji huazimwa kutoka Mamlaka na kufungiwa Mteja wakati wa kuunganishiwa maji kwa mara ya kwanza.** Mteja anapaswa kulipia gharama ya ukodishaji Dira ya Maji. Gharama halisi ya Dira ya Maji ni tofauti na gharama ya ukodishaji, hivyo kimsingi Dira ya Maji ni mali ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mjini Moshi na siyo mali ya Mteja.
- **Dira ya Maji ya Mteja itafungwa na Mafundi wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mjini Moshi tu wakati wa kumuunganishia Mteja huduma ya maji safi na si mtu mwingine yeoyote.**

- Mteja haruhusiwi kuifungua, kuitengeneza, kuihamisha mahali itakapofungwa na mafundi wa Mamlaka, kuichezea au kuruhusu watoto ama mtu mwingine yejote kuichezea na hatimaye kuiharibu Dira ya Maji iliyofungwa.
- Ikiwa Dira ya Maji itaharibiwa, Mteja atapaswa kulipia gharama za kununua Dira ya Maji nyingine kwa bei itakayokuwa inauzwa kwa wakati huo vinginevyo atalazimika kukosa huduma ya maji safi na salama.
- Mteja atapaswa kuhakikisha Dira ya Maji na viungio vingine vinavyoambatana nayo vinalindwa kutokana na kila aina ya uharibifu utakaoweza kutokea ili kuepuka hasara ya kulipia adhabu ya uharibifu wa Dira ya Maji.
- **Mteja analazimika kukubaliana na Masharti yaliyowekwa na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mjini Moshi juu ya Usimamizi na Ulinzi wa Dira ya Maji.**

Kwa Maelezo ama Matatizo yoyote juu ya Dira ya maji, Mteja atapaswa kuwasiliana na Kitengo cha Mahusiano na Wateja (Huduma kwa Wateja) cha Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mjini Moshi.

Tunza Dira Yako ya Maji ili Kuendelea Kupata Huduma ya Maji Safi na Salama!

**MKURUGENZI MTENDAJI
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA
MJINI MOSHI
S.L.P 324, MOSHI Simu: 2751164
Barua Pepe: muwasa@kilionline.com**